

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Kumb.Na. FA.634/12/02A/99

22/03/2018

TANGAZO LA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mbadala kwa Watendaji kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa chenye Kumb. CFC.26/205/01"FF"/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 kikisomwa pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha ajira mbadala kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa yenye Kumb.Na.CFC.26/205/01"GG/95 ya tarehe 12 Machi,2018 kutoka Ofisi ya Katibu Mkuu-Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa anawatangazia Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III- NAFASI 25

SIFA ZA MWOMBAJI:

Awe na Elimu ya kidato cha Nne (IV) au Sita(VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja wapo ya fani zifuatazo:

Utawala,Sheria,Elimu ya Jamii,Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo,Dodoma au Chuo chochote kinacho tambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III:

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
2. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao,kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
3. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
4. Katibu wa Mikutano ya kamati zote za Halmashauri ya Kijiji

5. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
6. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamamsisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
7. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji
8. Kusimamia ,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
9. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.


NGAZI YA MSHAHARA:

TGS B kuanzia shilingi 390,000 hadi 489,000 kwa mwezi. Mwajiriwa ataanza na mshahara wa Tsh.390, 000 kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA:

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi kwenye Kijiji chochote ndani ya Halmashauri ya Wilaya Kyerwa.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18-45.
3. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela
4. Maombi yote yaambatane na Wasifu wa mwombaji/CV)
5. Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma , cheti cha kuzaliwa na picha (passport size) zilizoandikwa jina la mwombaji nyuma
6. Testimonials "provisional results", "Results Slips", Kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA.**
7. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
8. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.
9. Waombaji walio wahi kuacha kazi, kuachishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha Kuajiriwa tena.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04 .04.2018 saa 9.30 Alasiri
11. Maombi yote yatumwe kwa:

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA
S.L.P 72
KYERWA**


**Shadrack M. Mhagama
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KYERWA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KYERWA**

Nakala : Mbao za Matangazo

: Tovuti ya Halmashauri – www.kyerwadc.go.tz